

Laini ya Msaada wa COVID-19 ya Wazee

Laini ya Msaada wa COVID-19 ya Wazee hutoa habari, inasaidia na inaunganisha kwa Waaustralia wakubwa.

Wazee wengine wako hatarini kwa COVID-19 lakini hawatumii mtandaoni na wanahitaji njia za kupata habari kwa hali zao. Laini ya Msaada wa COVID-19 ya Wazee hutoa habari na msaada.

Waaustralia wakubwa, familia zao, marafiki na walezi wao wanaweza kupiga SIMUBURE 1800 171 866 ikiwa:

- wangependa kuzungumza na mtu kuhusu vizuizi vya COVID-19 na athari zake kwao
- wanahisi upweke au wasiwasi juu ya mpendwa
- wanatunza mtu na wanahitaji habari fulani au mtu wa kuongea naye
- wanahitaji msaada au ushauri juu ya kubadilisha huduma za wazee wanazopokea
- wanahitaji msaada kupata huduma mpya za utunzaji au vifaa muhimu kama vile ununuzi
- wana wasiwasi juu yao wenyewe, rafiki au mtu wa familia anayeishi na Dementia
- wangependa kupanga ukaguzi wa ustawi wa mara ya moja tu au wa kawaida wa maisha yao, au mtu mwingine.

Waaustralia wakubwa, familia zao, walezi, marafiki wao au wasaidizi wanaweza:

- kupiga simu kwenye **1800 171 866**
- 2:30 asubuhi hadi 12 jioni (8.30am – 6pm AEST) siku za wiki
- kwa habari zozote au huduma wanazoweza kuhitaji.

Laini ya Msaada wa COVID-19 ya Wazee ni uvumbuaji wa pamoja:

- COTA Australia,
- Dementia Australia,
- National Seniors na
- OPAN,
- Kuungwa mkono na ufadhili kutoka Serikali ya Australia.

Msaada wa Huduma ya Ufasiri na Ukalimani (TIS)

Waaustralia wakubwa ambao hawasemi Kiingereza wanaweza:

- kupiga simu kwenye TIS Taifa kwenye 131 450,
- kuomba kwa mkalimani, na
- kuomba kuunganishwa na Laini ya Msaada wa COVID-19 ya Wazee au utamke nambari ya simu ya 1800 171 866 ili kuunganishwa.